



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI
(NACTE)



TAARIFA KWA UMMA

KUSITISHWA UDAHILI WA WANAFUNZI KATIKA MUHULA WA MACHI
KWA VYUO VYA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI KUANZIA MWAKA
WA MASOMO 2021/2022

Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) linapenda kuutaarifu umma kuwa udahili wa Machi umesitishwa. Udahili huo ulianza baada ya wadau mbalimbali, ikiwa ni pamoja na taasisi zinazotoa mafunzo kuomba kuwepo na dirisha dogo la udahili wa wanafunzi la mwezi Machi ili kuziba nafasi zinazobakia baada ya udahili wa mwezi Septemba kila mwaka kukamilika. Maombi haya pia yalilenga kuwapa fursa ya kujiunga na mafunzo waombaji wanaokosa nafasi katika udahili wa Septemba.

Tathmini ya Baraza kuhusu ufanisi wa udahili wa machi imebaini uwepo wa changamoto nyingi za kiutendaji zinazoathiri ubora wa taaluma kutokana na mpango huu. Changamoto hizo ni pamoja na;

1. Idadi ndogo ya wanafunzi wanaodahiliwa muhula wa Machi ikilinganishwa na wanafunzi wanaodahiliwa kwenye muhula wa Septemba imesababisha wanafunzi hawa wasipewe kipaumbele wakati wa ufundishaji;
2. Baadhi ya Vyuo kutokuwa na miundombinu na walimu wa kutosha kufundisha wanafunzi wa mihula yote miwili;
3. Baadhi ya vyuo kufupisha muda wa mafunzo kwa wanafunzi wanaodahiliwa muhula wa Machi;
4. Kwa upande wa Vyuo vya Afya, kumekuwepo na mwingiliano mkubwa wa ufundishaji na mafunzo kwa vitendo kwenye hospitali/vituo vya afya na kusababisha misongamano mikubwa ambayo huathiri si tu ubora wa mafunzo nchini bali pia huduma zinazotolewa na hospitali/vituo vya afya kwa wateja wake;
5. Kuwepo kwa ubadilishaji/uhamaji wa mara kwa mara wa wanafunzi kutoka muhula wa Machi kwenda muhula wa Septemba wakiwa mafunzoni bila ya kufuata utaratibu; na
6. Kuwadahili wanafunzi chuoni bila ya idhini ya Baraza hasa wale wanafunzi wa kidato cha Nne waliomaliza hivi karibuni wakisubiri kupangiwa mafunzo na Serikali.

Hivyo, Baraza linavitaarifu Vyuo vyote vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi nchini kuwa udahili wa Mwezi wa Machi (*March Intake*) **UMESITISHWA** rasmi kuanzia Mwaka wa Masomo 2021/2022. Vyuo vyote vitatakiwa kudahili mara moja tu (*September Intake*) kwa mwaka.

IMETOLEWA NA:

OFISI YA KATIBU MTENDAJI

BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI (NACTE)

TAREHE: 29/09/2021